JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 02/03/2022 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI

### 1.0 MAHUDHURIO

### 1.1 WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Pius Mwelase | Mwenyekiti H/W | Mwenyekiti |
| 2. | Mh. Jane Komba | M/Mwenyekiti H/W | Mjumbe |
| 3. | Mh. Severus Kamguna | Diwani Kata ya Igawa | Mjumbe |
| 4. | Mh. Bonaventure Kiwanga | D/Kata ya Kilosampepo | Mjumbe |
| 5. | Mh. Said Tira | D/Kata ya Malinyi | Mjumbe |
| 6. | Mh. Editha Makumba | D/V/ Ngoheranga | Mjumbe |
| 7. | Mh.Lucas Mgomahenga | Diwani Kata ya Sofi | Mjumbe |

### 1.1.3 WAKUU WA IDARA NA VITENGO

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Absalom Gepson | K/Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 2. | George Lazaro | K/Mkuu wa Idara ya Utumishi | Mjumbe |
| 3. | Godfrey Bisendo | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi | Mjumbe |
| 4. | Sarah Kibona | K/Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | Mjumbe |
| 5. | Omary Seif | Mratibu wa UKIMWI | Mjumbe |
| 6. | Martin Mhode | Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika | Mjumbe |
| 7. | Christina Sulley | Kaimu Katibu wa TSC | Mjumbe |
| 8. | Dr. Goodluck Mosha | K/Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Mjumbe |
| 9. | Subilaga Msyani | Mkuu wa Kitengo cha Sheria | Mjumbe |
| 10. | Emil Kalanga | Mkuu Kitengo cha Uchaguzi | Mjumbe |
| 11. | Richard Sanga | K/Mkuu wa Idara ya Mipango na Takwimu | Mjumbe |
| 12. | Sylivia S. Lussumo | Mratibu wa TASAF | Mjumbe |
| 13. | Frank Mganga | K/Mkuu Idara ya Maendeleo ya Jamii | Mjumbe |
| 14. | Dr. Azizi Ketto | K/Mkuu wa Idara ya Afya(W) | Mjumbe |
| 15. | Simon Nkwabi | K/Mkuu wa Idara ya Ujenzi | Mjumbe |
| 16. | Feddy Munyaga | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili | Mjumbe |
| 17. | James Msindo | K/Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari | Mjumbe |
| 18. | Rachel Mkumbwa | K/Mkuu wa kitengo cha Ugavi | Mjumbe |
| 19. | Severa Mrosso | K/Mkuu wa Idara Elimu Msingi | Mjumbe |
| 20. | Lightness Segesa | K/Mkuu Idara ya Mazingira | Mjumbe |
| 21. | Bernard Mbumbumbu | Afisa Afya | Mjumbe |

1.5 SEKRETARIETI

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Issa Matanda | Mwandishi wa vikao |
| 2 | Kimwana Mwatawala | Afisa Utumishi |

**KUMB.NA.01/03/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimtaarifu Mwenyekiti kuwa akidi ya wajumbe imetimia hivyo afungue kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kufika katika kikao na aliwaomba kushiriki kikao wakiwa huru katika kuhoji na kupata majibu yanayostahili.

Mwenyekiti alifungua kikao saa **10:19** jioni.

**KUMB.NA.02/03/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA.**

Wajumbe waliridhia agenda zifuatazo kujadiliwa katika kikao.

1. Kufungua kikao
2. Kusoma na kuridhia agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 08/01/2022
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe 08/01/2022.
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Januari, 2022.
6. Ombi la kuazima marumaru za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na Mabati 50 katika Kituo cha Afya Itete kwa ajili ya kujengea ujenzi wa Wodi tatu (3) Hospitali ya Wilaya.
7. Ombi la utekelezaji wa mradi wa jengo la dharula (EMD) na nyumba ya Watumishi (three in one)
8. Maombi ya kupitisha mitaji ya ruzuku ya wasichana balehe na wanawake vijana Tsh. **20,022,600/=** kutoka TASAF.
9. Ujenzi wa shule ya Sekondari mpya Kata ya Malinyi kupitia mradi wa SEQUIP.
10. Mabadiliko ya matumizi ya fedha.
11. Taarifa za zoezi la anuani za makazi.
12. Hali ya magari ya Halmashauri.
13. Mengineyo
14. Kufunga kikao.

Pia Diwani wa Kata ya Kilosa Mpepo aliongeza kwa kushauri menejimenti kutembelea kila shule shikizi kuangalia vifaa vilivyobaki na kukusanywa sehemu moja ili vitumike kwani bila utaratibu mzuri wa kuhifadhi vinaweza kutumika visivyo.

Kaimu Mhandisi wa Ujenzi alieleza kuwa hadi kuisha jengo la kutunzia dawa vitabaki vigae zaidi ya mia tano na jengo la Utawala litatumia vigae visivyozidi mia tatu (300) kwa hiyo vitabaki vigae mia mbili **(200)** hivi.

Kaimu Mhandisi wa Ujenzi alisema Kwa kuwa tunataka kumaliza haraka ujenzi wa wodi tatu **(3)** ili tuletewe fedha kwa ajili ya majengo mengine tunaomba kuazima kwani jengo la utawala haliwezi kuanza ujenzi sasa hivi hadi kupatikana kwa mapato ya ndani.

Kuhusu fedha zilizobaki za ujenzi wa Wodi tatu **(3)** hadi sasa kwenye akaunti kuna fedha kiasi cha **Tsh. 179,000,000/=** ambazo matumizi yake bado ikiwemo na ununuzi wa marumaru.
Aliwaondoa shaka wajumbe kwamba ujenzi wa majengo saba **(7)** utakamilika na vigae vitakavyokopwa vitarudishwa hivyo aliwaomba wajumbe kuridhia kuazimwa malumalu pamoja na mabati **50** kutoka Kituo cha Afya Itete ili kukamilisha ujenzi wa wodi tatu ifikapo tarehe **30/03/2022**.

Mjumbe toka Kata ya Kilosampepo (Mhe. Bonaventure Kiwanga) alitaka kujua juu ya kuchukuliwa bati hizo **50** wakati ujenzo unaendelea.

Kaimu Mhandisi wa ujenzi alieleza kuwa kazi ya kuezeka Kituo cha Afya Itete imekwisha na bati 56 zimebaki.

**HITIMISHO**
Wajumbe walichangia hoja kwa muda mrefu akiwemo pia Diwani wa Kata ya Sofi (Mhe. Lucas Mgomahenga), na wote kwa pamoja waliridhia kuazimwa kwa vifaa tajwa hapo juu na kutaka virudishwe kwa wakati. Kama ilivyoomba na wajumbe wajulishwe kurudishwa kwa vifaa hivyo.

**KUMB.NA.07/03/2022: OMBI LA UTEKELEZAJI WA MRADI WA JENGO LA DHARULA (EMD) NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE)**
Kaimu Mhandisi wa Ujenzi aliwasilisha ombi tajwa hapo juu, kwamba zabuni ilitangazwa, watu wameweka gharama kubwa ukilinganisha na fedha zililetwa toka Serikali Kuu yaani **(300,000,000/=)** jengo la dharula na **90,000,000/=** nyumba ya Watumishi (Three in one).

Amekuja Mkadiria Majengo (QS) kwa kumuazima toka Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga Mkadiria Majengo amekadiria zaidi ya **Tsh. 427,000,000/=** jengo la dharula na **157,246,920.00/=** zaidi **Tsh. 69,246,368.40/=** jengo la watumishi (Three in one).

Aliomba idhini ya kuanza kwa njia ya **Force Akaunti** kama walivyotoa mwongozo mpya, toka TAMISEMI wa kutumia njia hiyo ya ujenzi.

Wajumbe waliungana na menejimenti wa kuanza kwa ujenzi, aidha walishauri wakati wa kuwasilisha taarifa iwasilishwe na Miongozo toka TAMISEMI au maeneo mengine yanayohusika.

Aidha, walitaka kujua kiasi kilichoongezeka na kama Halmashauri ina uwezo wa kumalizia kama ujenzi utaanza.

Kaimu Mhandisi Ujenzi alieleza kuwa ujenzi utaanza kwa fedha iliyopo majengo yatakapofikia itaombwa fedha Serikali Kuu ya kukamilisha ujenzi.

**HITIMISHO**
Wajumbe walipokea na kupitisha ombi la kuendelea na ujenzi wa majengo tajwa hapo juu.

**KUMB.NA.08/03/2022: MAOMBI YA KUPATIWA MITAJI YA RUZUKU YA WASICHANA BALEHE NA WANAWAKE VIJANA TSH. 20,022,600.00/= KUTOKA TASAF.**
Kaimu Mratibu wa TASAF Wilaya aliwasilisha ombi la kupitisha Tshs.20,022,600/= kwa ajili ya mtaji kwa Wasichana balehe na Wanawake Vijana kutoka kaya za TASAF.

Ombi lilionyesha kuwa Tume ya kudhibiti UKIMWI kupitia mfuko wa Dunia na kushirikiana na Wadau mbalimbali wameona namna ya vijana hao watakavyojikimu kimaisha wakiwa salama bila kupata VVU na UKIMWI.

Vijana 176 wamepata mafunzo kutoka vijiji 16 vya mpango wa TASAF na kupata mafunzo ya ujasilia mali kati yao vijana 169 ndio walikidhi vigezo vya kupata ruzuku kupitia mipango yao ya Biashara.

Aidha, mipango 78 kati ya 169 imefanikiwa kufungua akaunti benki ya NMB yenye thamani ya Tshs. 20,022,600/=.

**MAJADILIANO**
Mjumbe mmoja alitaka kujua kama fedha, wanazopewa zina riba. Aidha, Mratibu wa TASAF alijibu kuwa ni fedha hizo Ruzuku ya msaada kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Mjumbe mwingine alitaka kujua vigezo vilivyotumika kupata wahusika.

Mratibu wa TASAF alieleza kuwa ni orodha iliyotoka yaTASAF Makao Makuu na kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

Mjumbe mwingine tena alishauri madiwani washirikishwe kupata uelewa katika vitu mbalimbali kwani ni viungo muhimu katika kutoa maamuzi.

Aliomba idhini ya kuanza kwa njia ya **Force Akaunti** kama walivyotoa mwongozo mpya, toka TAMISEMI wa kutumia njia hiyo ya ujenzi.

Wajumbe waliungana na menejimenti wa kuanza kwa ujenzi, aidha walishauri wakati wa kuwasilisha taarifa iwasilishwe na Miongozo toka TAMISEMI au maeneo mengine yanayohusika.

Aidha, walitaka kujua kiasi kilichoongezeka na kama Halmashauri ina uwezo wa kumalizia kama ujenzi utaanza.

Kaimu Mhandisi Ujenzi alieleza kuwa ujenzi utaanza kwa fedha iliyopo majengo yatakapofikia itaombwa fedha Serikali Kuu ya kukamilisha ujenzi.

**HITIMISHO**

Wajumbe walipokea na kupitisha ombi la kuendelea na ujenzi wa majengo tajwa hapo juu.

**KUMB.NA.08/03/2022: MAOMBI YA KUPATIWA MITAJI YA RUZUKU YA WASICHANA BALEHE NA WANAWAKE VIJANA TSH. 20,022,600.00/= KUTOKA TASAF.**

Kaimu Mratibu wa TASAF Wilaya aliwasilisha ombi la kupitisha Tshs.20,022,600/= kwa ajili ya mtaji kwa Wasichana balehe na Wanawake Vijana kutoka kaya za TASAF.

Ombi lilionyesha kuwa Tume ya kudhibiti UKIMWI kupitia mfuko wa Dunia na kushirikiana na Wadau mbalimbali wameona namna ya vijana hao watakavyojikimu kimaisha wakiwa salama bila kupata VVU na UKIMWI.

Vijana 176 wamepata mafunzo kutoka vijiji 16 vya mpango wa TASAF na kupata mafunzo ya ujasilia mali kati yao vijana 169 ndio walikidhi vigezo vya kupata ruzuku kupitia mipango yao ya Biashara.

Aidha, mipango 78 kati ya 169 imefanikiwa kufungua akaunti benki ya NMB yenye thamani ya Tshs. 20,022,600/=.

**MAJADILIANO**

Mjumbe mmoja alitaka kujua kama fedha, wanazopewa zina riba. Aidha, Mratibu wa TASAF alijibu kuwa ni fedha hizo Ruzuku ya msaada kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Mjumbe mwingine alitaka kujua vigezo vilivyotumika kupata wahusika.

Mratibu wa TASAF alieleza kuwa ni orodha iliyotoka yaTASAF Makao Makuu na kupitia Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

Mjumbe mwingine tena alishauri madiwani washirikishwe kupata uelewa katika vitu mbalimbali kwani ni viungo muhimu katika kutoa maamuzi.

**HITIMISHO**
Wajumbe walipokea na kupitisha taarifa ya hali ya magari ya halmashauri.

**KUMB.NA.13/03/2022: MENGINEYO**
Wajumbe walishauri suala la kufuata ratiba ya vikao lizingatiwe

Pia Menejimenti kuona uwezekano wa kuweka mfumo wa genereta chumba kimoja, ili umeme ukikatika kazi za Serikali ziendelee.

Vile vile walishauri taarifa ya Idara ya Utumishi na Utawala iwe inawasilisha taarifa zake kila mwezi hasa zile zinazotekelezwa kila mwezi angalau kwa ufupi.

Katibu alieleza kuwa ushauri wa wajumbe utazingatiwa.

**KUMB.NA.14/03/2022: KUFUNGA KIKAO**
Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikao vizuri na kuitaka Menejimenti kuzingatia ushauri uliotolewa na wajumbe.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 1:44 usiku.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA**

| | |
|---|---|
| **Saini:**.............................. | **Saini:** Kaniba......... |
| **Jina:** JOANFAITH KATARAIA | **Jina:** JANE OKOMBA |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| **Tarehe:** 19/03/2022 | **Tarehe:** 19/03/2022 |